# UQAB

Jarida la



*Toleo 36 - Jamada I 1441 H / Januari 2020 Miladi*

**Waislamu Warohingya wanaingia Mwaka Mpya wakiwa na hofu**

**Je Nchi za Afrika ni Nchi za Kimfumo?**

**Serikali za Kisekula Zimebadilisha Majanga ya Kimaumbile kuwa Mgogoro**

**Mwamko wa Kiislamu Utaletwa na Khilafah Pekee**

**Ahadi Tupu kwa Wanawake wa Afghan**

**SWALI/JAWABU: Harakati za Kiraia Nchini Iraq, Lebanon na Iran**



## Msimamo wa Kiislamu juu ya Ripoti ya BBI

# Msimamo wa Kiislamu juu ya Ripoti ya BBI



Mnamo Jumatano, 27 Novemba 2019, Wakenya walishuhudia uzinduzi rasmi wa ripoti ya BBI kutoka kwa Rais Uhuru Kenyatta ndani ya Bomas huko Nairobi. Tukio hilo lilikuwa ni kilele cha mkono wa kheri baina ya Rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga mnamo 9 Machi 2018 uliofanyika Harambee House. Kabla ya mkono wa kheri, Kenya ilikuwa ndani ya mzozo wa kiuchaguzi uliohusisha muungano wa upinzani NASA ukiongozwa na Raila Odinga na Chama cha Jubilee kikiongozwa na Uhuru Kenyatta. Licha ya kwamba uchaguzi wa urais uliofanyika mnamo 8 Agosti 2017 ulibatilishwa na kuagizwa ufanywe upya na Mahakama ya Upeo ya Kenya mnamo 1 Septemba 2017. NASA ilikataa kushiriki na kujiepusha na uchaguzi wa marudio uliofanyika mnamo 17 Oktoba 2017 ambapo Chama cha Jubilee kilishiriki na kutangazwa mshindi. Sababu kubwa ya NASA kujiepusha na uchaguzi huo ni kwamba matatizo yaliyotajwa kuwa ndio sababu ya kubatilishwa uchaguzi yalikuwa hayaja suluhishwa na yalijumuisha usimamizi mbaya wa uchaguzi ambao ulitakiwa kufanyiwa mabadiliko IEBC na kuuondoshwa kwa miswada ya mabadiliko ya uchaguzi iliyokuwa imewasilishwa bungeni na utawala wa Jubilee.

Kilichofuatia baada ya uchaguzi wa marudio mnamo Jumanne, 17 Oktoba 2017 ilikuwa ni machafuko ya kila wiki na ukosefu wa usalama yalizozidi kwa kuapishwa kwa Raila Odinga mnamo 30 Januari 2018, nchi ilikuwa inakaribia kutotawalika na wasiwasi ulikuwa juu hususan mji mkuu Nairobi ilhali wawekezaji wakihofia maisha yao na uwekezaji wao! Hivyo basi, kama ilivyotokea mnamo 2007/8 wahusika wakuu walikutana Harambee House na kupeana mikono kutoka wakati huo wasiwasi ulipotea, wandani wa Raila wakateuliwa katika mashirika ya serikali miongoni mwa vyeo vingine! Zaidi ya hayo, mnamo Mei 2018 tumekazi ya BBI ikasajiliwa rasmi katika gazeti la serikali na kupewa kazi ya kutafuta maoni ya mwelekeo gani bora kuhusiana na kutatua matatizo yanayowakabili Wakenya na kuwasilisha ripoti kwa Rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga. Kwa kuongezea, amani na usalama ilirudi ilhali wawekezaji na uwekezaji wao wakahisi salama chini ya mchakato mpya wa kisiasa kiasi kwamba tukashuhudia ziara ya kipekee ya Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Theresa May mnamo Alhamisi, 30 Agosti 2018 ndani ya miaka 30 tangu ziara ya Margaret Thatcher nchini Kenya. Kwa mara nyingine Waziri Mkuu wa zamani aliwapongeza Raila na Uhuru kwa kutanguliza maslahi ya nchi kwanza na kudhamini usalama wake.

Hivi sasa nchi inakodolea mzunguko mpya wa mzozo huku wengine wakitaka ripoti ya BBI kupelekwa bungeni ili kuboreshwa zaidi na kutekelezwa. Upande wa pili, tunao wengine wanaotaka kura ya maoni ili ripoti ipitishwe na kutekelezwa. Na katika mchakato huu ndipo Waislamu wamejipata njia panda ima kuikubali ripoti na kufuata njia ya bungeni au kura ya maoni pasina kuzingatia ima wameisoma ripoti au la.

Baada ya kutathmini kwa kina matukio hayo hapo juu haina shaka kwamba ripoti ya BBI ni nakala iliyotungwa na wanadamu ambayo asili yake ni akili iliyo na kikomo na SIO wahyi. Kwa kuongezea, ni nakala iliyopindishwa ili kuwahadaa na kuwatuliza watu walale hususan

***Endelea Uk..3***



**Email: info@uqab.or.ke**

kipindi hichi ambapo Wakenya wanataabika kwa kuishi katika hali za kukatisha tamaa! Kenya ni dola ya kisekula ambayo itikadi (aqeedah) yake ni usekula (kutenganisha dini na maisha na dola) na mfumo wake wa kirasilimali unachipuza kutokana na kipaumbele cha uhuru wa kumiliki (uchumi) kwa hiyo unapima vitendo vya mwanadamu kwa msingi wa maslahi na manufaa. Kwa kuongezea, Kenya hadi sasa ni shamba la kikoloni ambalo viongozi (mameneja wa shamba) wake wameuza nafsi zao kwa mabwana zao Wamagharibi wakoloni na hivyo kipaumbele chao ni kuwa watumwa kwao na hivyo sera na sheria wanazozitunga ni kwa ajili ya kuwamakinisha wao na maslahi yao kwa gharama za raia wa kawaida!

Kama Waislamu sisi ni watumwa wa Mwenyezi Mungu (swt) na kufaulu kwetu ni kumridhisha Mwenyezi Mungu (swt) pekee kupitia kujisalimisha kwetu katika maamrisho na makatazo Yake (swt) kwa msingi wa kipimo cha halali na haramu. Itikadi yetu ni: **“لا إله إلا الله محمد رسول الله” “Hapana mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu”** Kwa msingi wa itikadi yetu ni lazima tujifunge na Qur’an na Sunnah pekee. Mwenyezi Mungu (swt) asema: **“يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ” “Enyio mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume” [An-Nisa: 59], “إِنِ ٱلۡحُكۡمُ إِلَّا لِلَّهِۚ” “Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mung tu” [Yusuf: 40], “وَمَنۡ أَحۡسَنُ مِنَ ٱللَّهِ حُكۡمٗا” “Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu” [Al-Maidah; 50]** na **“فَإِن تَنَٰزَعۡتُمۡ فِي شَيۡءٖ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ” “Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume” [An-Nisa: 59].** Kwa hiyo ripoti ya BBI ni natija ya mzozo wa kisiasa uliosababishwa na uchaguzi unaokwenda kinyume na Uislamu. Kenya kama ulivyo utawala wowote wa kisekula inajivunia kuwa ni dola ya kidemokrasia kwa maana kwamba raia wanatunga, wanarekebisha na kufutilia mbali sheria ili kusimamia maisha yao kwa maana nyingine ni kuwa ubwana ni wa watu na watu ndio chimbuko la mamlaka kwa maana nyingine wanaweza kumchagua mwanamke au mwanamume kama mtawala/kiongozi wao na wanaweza kumuondosha wakati wowote wanapohisi kuwa hawakidhii maslahi au manufaa yao! Hii ni **KINYUME** na Uislamu ambapo ubwana ni wa Mwenyezi Mungu (swt) pekee kupitia Shari’ah Yake (Qur’an na Sunnah) na mamlaka ni ya watu (Ummah) lakini punde wanapomchagua Khalifah/mtawala/mwanamume hawezi kuondoshwa mpaka pale atakapotenda/kudhihirisha *Ukafiri* wazi.

Kwa mujibu wa hayo hapo juu ni wazi kwamba ripoti ya BBI haiwahusu Waislamu. Kwa kuwa msingi wake ni mfumo wa kisekula wa kirasilimali ambao kutokana nao zimechipuza nidhamu zake zenye sumu kama vile demokrasia, mujtama wa kihuria, nidhamu ya kiuchumi ya ukandamizaji, sera ya kigeni kwa msingi wa ukoloni n.k. Kwa upande mwingine, Waislamu lazima warudie Uislamu wao kimfumo kwa kuwa una suluhisho ya matatizo yote yanayowakumba wanadamu duniani kote na yaliyo sababishwa na mfumo batili wa usekula wa urasilimali na nidhamu zake. Kuurudia kwao lazima kuanzie pale ambapo Mtume (saw) alipokuwa mtume mnamo 610 M na maisha yake na maswahaba zake (ra) yalikuwa mabaya na yaliyojaa changamoto kama tunayokumbana nayo sasa nchini Kenya na duniani kote. Lakini kila kitu kikabadilika mnamo 622 M pale ambapo Mtume (saw) na maswahaba zake (ra) walipohama Makkah kwenda Madinah na aliwasili kama mtawala na kuasisi Dola ya Kiislamu ya kwanza duniani, alipofariki (saw) mnamo 632 M, Abu Bakr (ra) akachukua utawala kama Khalifah/mtawala wa kwanza mpaka Khalifah wa mwisho (102) Abdulmaji II mnamo 1924 M. Katika kipindi chote hicho cha takribani karne kumi na tatu chini ya utawala wa Dola ya Kiislamu ikitawala kwa Shari’ah, Waislamu na wasiokuwa Waislamu na wanadumu jumla walishuhudia utulivu, amani na ustawi ambao haujawahi kushuhudiwa katika mgongo wa ardhi.

Tangu kuvunjwa kwa Khilafah mnamo 3 Machi 1924 M, Waislamu wamekuwa mayatima ambao damu zao zinamwagwa pasina huruma na mali zao kuporwa kilafi na maadui wa Uislamu na Waislamu ambao leo wanaongozwa na Amerika na washirika wake duniani. Khilafah ya Waislamu ambayo ilikuwa dola moja chini ya mtawala mmoja anayetawala kwa Shari’ah iligawanywa na kuwa vijidola 50+ vilivyokadhibiwa watawala wajinga (ruwaibidha) waliouza nafsi zao kwa mabwana zao Wamagharibi wakoloni kwa usaliti wao wa kuivunja Khilafah. Kwa hiyo **suala msingi kwa Waislamu leo** la kuwashughulisha, ni kufanyakazi ya kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Dola ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Ni kupitia Khilafah pekee ndipo Waislamu na wanadamu jumla watapata utulivu, amani na ustawi mambo ambayo yanaahidiwa na ripoti ovu ya kisanii ya BBI ambayo nia yake ni kudumisha mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zinazonuka ambazo ndio chanzo cha wanadamu kutaabika nchini Kenya na duniani.

Hivyo basi, Waislamu lazima wajiepushe na mijadala isiyokuwa na natija kuhusiana na ripoti ya BBI na badala yake wajiunge na ndugu zao wa Hizb ut Tahrir kufanya kazi pasina kuchoka katika ulinganizi wa Khilafah na wakati huo huo kufanya mijadala yenye natija inayolenga kupambana na mzizi unaosababisha tabu kwa wanadamu unaojumuisha namna ya kuondosha mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake fisadi na kuweka Uislamu na nidhamu zake tukufu zinazochipuza kutoka kwa Muumba (swt). Hakika, ulinganizi wa Khilafah ndio ulinganizi pekee wenye kuleta mageuzi ya kikweli na kimsingi ambayo kila mtu kutoka Mashariki kwenda Magharibi anayalilia.

**“وَيَوۡمَئِذٖ يَفۡرَحُ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ” “Na siku hiyo Waumini watafurahi” [Ar-Rum: 4]**.

**Ali Nassoro Ali**

# HABARI & MAONI
# Waislamu Warohingya wanaingia Mwaka Mpya wakiwa na hofu kwa kukosekana Khilafah

**Habari:**

BBC iliripoti kuhusiana na kupambamoto kwa janga la Rohingya huku idadi ya wanaotarajiwa kushtakiwa dhidi ya serikali ya Myanmar ikiwasilishwa katika mahakama za kimataifa na Venezuela na Gambia. Habari iliyotoka mnamo 19 Novemba 2019 inaelezea hadithi kwamba kijana wa miaka 11 anayeitwa Omar anayeishi pasina familia yoyote katika kambi ya wakimbizi ya Cox Bazaar ndani ya Bangladesh. Mamake na babake waliuliwa kinyama na wanajeshi wa Myanmar na kila siku huamka na kulia akikumbuka kuwapoteza wazazi wake wapendwa. Kaka zake watatu na dada zake wawili nao pia waliuliwa katika msururu wa usafishaji kabila.

**Maoni:**

Mnamo Septemba 2018, wachunguzi wa UN walihitimisha kwamba majenerali wa Myanmar wanastahiki kufikishwa kizimbani kutokana na vitendo vyao dhidi ya Waislamu wa Jimbo la Rakhine ambapo zaidi ya Warohingya 700,000 walifurushwa ndani ya Bangladesh. Lakini mpaka wa leo hakuna hata afisaa mmoja aliyefikishwa mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC). Huku udhuru unaotolewa kwa kukosekana kupatikana kwa haki unaelezewa na Laetitia van den Assum ambaye ni mwanachama wa tume huru kuhusiana na hali ya Rakhine ikiongozwa na Katibu wa Kudumu wa zamani wa UN – Kofi Annan. Nukuu kuhusiana na kukosekana ufuatiliaji ni kama ifuatavyo; “Ni kweli maendeleo yanaweza kuwa polepole, lau utakuwa na cheo katika uongozi mkuu utalindwa, hakuna atakayekupeleka Hague.” Suala jingine lenye kuleta tashwishi ni kwamba Mshindi wa Tuzo ya Nobel Aung San Suu Kyi anatumia ngao ya kutohusika na kwamba kikatiba hana udhibiti wa jeshi. Mauaji ya kila siku ya wanaume, wanawake na watoto wasiokuwa na hatia yataendelea tukiingia mwaka mpya pasina kusitishwa na mamlaka yoyote kwa kuwa mahakama hizi za kimataifa za uhalifu zipo tu kuwahesabu watu binafsi fulani na zinahudumikia malengo na ajenda za kimagharibi. Tukizingatia kwamba serikali za kimagharibi zinaruhusu biashara zao kufanyika na Myanmar na kutengeza mabilioni katika faida inathibitisha kutowajibika kiukamilifu katika kuwasaidia Waislamu wa Myanmar. Uwepo wa kiongozi wa kweli wa Kiislamu kwa sura ya Khilafah itakuwa ndio umbile pekee ambalo halitokubali Warohingya kutaabika huku na kule duniani au kutiwa korokoroni katika kambi kama wanyama. Ilhali viongozi Waislamu duniani wameamua kusahau tabu nzito zinazoukumba Ummah, Mwenyezi Mungu (swt) hatosahau kujitoa muhanga kutokana na Iman. Tunawaombea mashahidi na wale watakaokuja wakiwa washindi katika Maisha ya Akhera na wale wanaoingia mwaka mpya huku wakiwa na hofu tukumbukeni Ayah hii katika Qur’an kuhusiana na subra wakati wa mitihani.

ٌديِعَسَو ٌّيِقَش ْمُهْنِمَف ِهِنْذِإِب ّالِإ ٌسْفَن ُمّلَكَت َال ِتْأَي َمْوَي

**“Na subiri, kwani Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanao fanya wema.” [Hud: 115]**

Je ni mayatima wangapi wanatakiwa kuwepo kama Omar, ni wangapi wapo lakini hawajaorodheshwa na wanatumiwa kutoka Syria, Iraq, Palestina, Afghanistan, Yemen na kwingineko? Tunawalingania Waislamu duniani kote kutumia njia zozote walizo nazo kunusuru na kufanyakazi ya kuishi chini ya Nidhamu ya Kisiasa ya Kiislamu na kujipatia nafasi miongoni mwa waliofaulu Kesho Akhera.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Imrana Mohammad**

# Je Nchi za Afrika ni Nchi za Kimfumo?

Ni bayana kuwa nchi zote za Afrika, katika katiba zao zadai kuwa ni nchi zinazotekeleza itikadi (aqeedah) ya kisekula (kiilmaniya) yaani mfumo wa kimaisha wa kirasilimali. Je kunukuliwa kwa mfumo wa kirasilimai katika katiba ya tosha kudai kuwa nchi za Afrika ni za kimfumo?

Ili tuweze kupata jawabu, hapana budi kufahamu nukta mbili zifuatazo:

**Kwanza,** mfumo kwa mujibu wa Sheikh Taqiuddin Nabahani katika kitabu chake cha Nidhamu ya Uislamu, asema kuwa mfumo ni, "Itikadi ya kiakili inayozaa nidhamu..." Huku itikadi ikimaanisha suluhisho juu ya matatizo ya mwanadamu ilhali nidhamu ikimaanisha namna ya kutekeleza, kuhifadhi na kueneza suluhisho hizo. Ama mfumo utabakia uko hai iwapo kuna watu wanauamini na kuutekeleza kwa khiyari pasina msukumo wa kinguvu wa serikali. Kupitia maana hii tunapata kwamba mifumo iliyopo hai leo ni miwili yaani wa Kirasilimali na Kiislamu.

**Pili,** nchi hutambulika ni ya kimfumo iwapo ina sifa zifuatazo:

a) imesimama juu ya kuamini pasina kushurutishwa wala kulazimishiwa itikadi maalumu ambayo ndiyo inayozaa nidhamu na ndio msingi wa fikra jumla ya usimamizi wa mambo ya watu.

b) itikadi hii iwe ndio chimbuko la sera (siasa) ya ndani na nje ya nchi. Ama kuhusu umbo na taasisi mbali mbali za dola, pia ziundwe kwa misingi ya itikadi hino. Isitoshe, itikadi ndio iwe ni yenye kufafanuwa namna ya kutekeleza sera za nchi.

c) malengo ya sera ya nje ya nchi iwe ni kwa ajili ya kueneza itikadi hiyo pamoja na kuhifadhi maslahi yake.

Kutokana na vigezo viwili hivyo hapo juu, ni bayana kuwa nchi za Afrika hazijafika kiwango cha kutambuliwa kuwa ni za kimfumo licha ya kunukulu ndani ya katiba zao mfumo wa kirasilimali.

Hakika lau raia wa nchi za Afrika wataachiwa pasina kutenzwa nguvu kuamua iwapo wanataka mfumo wa kisekula wa kirasilimali, wengi wao watautupilia mbali. Historia yaonyesha kuwa itikadi hii ya kisekula ni ya kulazimishwa juu yao kwa mabavu. Waenezaji mfumo, yaani nchi za kimagharibi kwa kweli hawakuwa na nia ya kuzifanya nchi za Afrika ni za kimfumo badala yake walizichorea sera pana kuhakikisha kuwa zinadumu kujisalimisha kwao kama dola asili za kimfumo. Hii ni kumaanisha kuwa nchi za bara Afrika ziwe ni zenye kuegemeza sera zake za ndani na nje kwa mujibu wa dola za kikoloni ambazo asili yake ni za kimfumo.

Hivyo basi nchi za Afrika sio nchi za kimfumo na badala yake ni makoloni ya dola za kimfumo. Zitaendelea kubakia kuwa mashamba ya kikoloni na watumwa kwa wakoloni Wamagharibi mpaka pale ambapo kutasimama tena dola ya Kiislamu ya kimfumo ambayo italikomboa bara la Afrika katika makucha ya masekula warasilimali wakoloni na kuwapa hadhi watu wake na kufurahia utajiri wao waliobarikiwa na Mwenyezi Mungu (swt) na hatimaye kuepukana na jinamizi la ukoloni!

**Khamisi Mwangemi (Abu Leila)**

# HABARI & MAONI
# Serikali za Kisekula Zimebadilisha Majanga ya Kimaumbile kuwa Mgogoro

**Habari:**

Wiki kadhaa zilizopita mvua nyingi iliweza kunyesha nchini na vyombo vya habari vimeripoti kuzidi kwa hali mbaya na vifo nchini kote ikijumuisha maeneo ya Kati, Pwani na Kaskazini mashariki huku wajuzi wakitoa ilani ya kukithiri kwa hali mbaya. Tukio la hatari zaidi la hivi majuzi ni kufariki kwa watu 50 huko Pokot Magharibi kutokana na mafuriko yaliyo haribu nyumba na kusababisha maporomoko ambayo yaliwazika wakaazi, kwani lililkuwa tukio hatari zaidi la kimaumbile ndani ya miaka ya hivi karibuni.

**Maoni:**

Mvua zimefichua kwa mara nyingine Serikali za Kisekula kukosa uwezo wa kusimamia majanga. Vifo vya huko Pokot Magharibi vingelipunguzwa kwa kuwepo maandalizi ya mikasa. Ni jambo la kushangaza kwamba siku kadhaa baada ya mkasa huo watu hawajaweza kuhesabiwa na hivyo kudaiwa kuwa wamekufa. Lakusikitisha zaidi maafisa wakuu serikalini wakiongozwa na Waziri wa Ndani Fred Matiang'i hawakuweza kufika katika kijiji ambako watu waliweza kufariki kinyama. Hali isingelifikia kiwango hicho lau serikali ingelikuwa imejiandaa na kuchukua hatua za mapema.

Kutokana na kukosekana sera ya nyumba za serikali na uporaji wa ardhi kutoka kwa maafisa wa serikali; familia nyingi masikini zimejipata hazina ardhi salama za kuishi na hivyo kuhatarisha maisha yao kwa kujenga katika sehemu ambazo zina mafuriko. Mpangilio mbaya wa barabara hususan katika maeneo ya ndani ndani hazijengwi kudumu kwa sababu ya ufisadi ambao umewafanya watu asilimia 32 kuishi katika maeno yaliyo na kilomita mbili za barabara za msimu na hili linazidisha hali mbaya wakati mafuriko yanapotokea kwa kuwa waathiriwa huwa hawana lakufanya.

Janga hili kiuwazi linaonyesha namna tawala za kirasilimali zinavyo badilisha mikasa na kuwa migogoro ya kibinadamu. Aghalabu mara nyingi mikasa hiyo inapotokea, inadhihirisha umbile la kweli la urasilimali na nidhamu zake tawala ambazo hazipeani kipaumbele kwa maslahi ya umma. Katika kinyang'anyiro cha uongozi, wanasiasa masekula warasilimali huzurura nchi yote kwa ndege wakitafuta kura lakini wakati wa mafuriko wanatizama kupitia runinga ilhali umma unazama! Hiyo ndiyo sura kamili ya urasilimali na viongozi wake ambao wanathamini tu maisha yao na hawayapi umuhimu maisha ya walalahoi.

Hata kama ni kweli mwanadamu hawezi kuzuia mikasa ya kimaumbile, lakini Mwenyezi Mungu (swt) amemuamrisha mwanadamu huyo kuchukua tahadhari za mapema kwa kuweka mipango kabambe kama njia ya kupunguza athari ya mikasa itakayotokea. Kama nidhamu kamili, Uislamu unaliweka jukumu la kusimamia mambo ya umma kwa serikali na sio watu binafsi. Mtume (saw) alisema: «الإِمَامُ رَاعٍ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ» **"Kiongozi wa watu ni mchungaji na atahesabiwa juu ya raia wake."**

Dola ya Kiislamu, al-Khilafah imepewa jukumu la kuhifadhi maisha ya raia wake wakati wote. Ama kuhusiana na mikasa kama mafuriko na maporomoko, Khilafah itatumia fedha zilizoko katika hazina (Baitul Mal) ili kuwasimamia walioathirika na jukumu lake juu kwa umma sio fadhla. Lau itakuwa hakuna fedha katika hazina, basi Khalifah atalazimika kuwatoza matajiri kiwango maalumu cha kodi ili kutatua tatizo hilo. Hivi ndivyo Khilafah inavyotarajiwa kuyalinda maisha adhimu ya raia wake bi idhni Ilah Taala.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Pakistan**

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 27/1441 Ijumapili, 11 Rabi ul Thani 1441 H 08/12/2019 M

# Mwamko wa Kiislamu Utaletwa na Khilafah Pekee, Kwa hiyo Watu wenye Nguvu Wajitokeze na Nussrah yao kwa ajili ya Khilafah kwa Njia ya Utume

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Mjadala umetanda ndani ya mitandao ya kijamii nchini Pakistan kuhusiana na video kupitia twitter kutoka kwa mwanajeshi mkuu wa majeshi ya majini akilingania Uislamu kutawala dunia. Admiral Zafar Mahmood Abbasi alitangaza kwamba Pakistan inaweza kuwa ndio kianzio cha kurudi kwa utukufu wa Uislamu, na kuongezea kwamba Waislamu walitawala dunia kupitia Uislamu, ilhali Ulaya ilitawala dunia kupitia kuipinga dini. Hakika, mwito wa kutawala kwa Dini ya Ukweli ndio hitajio maarufu la Waislamu, ikijumuisha wale walioko ndani ya jeshi. Lakini, watawala walioko lazima wasiruhusiwe kuelekeza kombo hisia za Kiislamu ili kutoa mwanya kwa Demokrasia, kwa kulingania sura yake mpya ima ni ya kiubunge, kiurais au nyingineyo. Mwenyezi Mungu (swt) ametuonya,

**(وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ)**

“Wala msichanganye kweli na uwongo na mkaificha kweli nanyi mnajua.” [Al-Baqarah 2:42]

Enyi Maafisa wa Majeshi ya Pakistan! Nguvu za kijeshi ambazo Mwenyezi Mungu (swt) amewapa, zinawapa uwezo wa kuifanya Pakistan kuwa ndio kianzio cha kurudi kwa Uislamu kama mwenendo wa maisha. Izikeni maiti inayonuka ya Demokrasia kwa kutoa Nussrah kwa Hizb ut Tahrir ili isimamishe Khilafah kwa Njia ya Utume. Tumieni nguvu zenu kuisimamisha dola yenye katiba ambayo kila kipengee chake kina dalili kutoka katika Qur’an na Sunnah. Simamisheni dola itakayofanyakazi ya kuunganisha Ardhi za Waislamu kuwa dola moja, badala ya kuzigawanya na kuzidhoofisha kwa mujibu wa mchoro wa mataifa ya Wamagharibi. Itoeni Nussrah yenu kwa uongozi wa Kiislamu ambao utapambana na ukandamizaji kwa nguvu za kijeshi kinyume na mazungumzo mezani, post za twitter na makubaliano. Mwageni damu zenu kupitia silaha zenu kwa kuilinda dola inayozikusanya rasilimali za Waislamu ili kulinda ustawi wa raia wote wa Dola kinyume na kuzisalimisha rasilimali hizi ili zitumiwe na wakoloni.

Hakika, Khilafah sio chaguo tu miongoni mwa machaguo, ni faradhi juu yetu sote, ambayo kuitelekeza imefungwa kuwa ni moja katika vifo vibaya, kufa pasina Uislamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema, **«مَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً»** “Yeyote atakayekufa pasina ahadi ya utiifu shingoni mwake amekufa kifo cha Jahilliyah.” (Muslim). Na Khilafah ni faradhi juu yetu katika kila zama na ambayo Mtume (saw) alisema kuihusu:

**«وَإِنَّهُ لَا نَبِيَّ بَعْدِي وَسَتَكُونُ خُلَفَاءُ فَتَكْثُرُ» قَالُوا: فَمَا تَأْمُرُنَا؟ قَالَ: «فُوا بِبَيْعَةِ الْأَوَّلِ فَالْأَوَّلِ وَأَعْطُوهُمْ حَقَّهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ سَائِلُهُمْ عَمَّا اسْتَرْعَاهُمْ»**

“Hakuna Mtume baada ya mimi, lakini kutakuwepo Makhalifa. Wakauliza, “Watuamrisha tufanyeje? Akajibu, “Wapeni ahadi ya utiifu mmoja baada ya mwengine, kwani Mwenyezi Mungu atawauliza kuhusu amana Aliyowapa.” (Bukhari) Kwa hiyo simamisheni zama mpya ya utawala wa Uislamu kupitia Nussrah yenu, ili mpate radhi za Mwenyezi Mungu (swt).

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Pakistan**

# Ahadi Tupu kwa Wanawake wa Afghan



Ujumbe wa Afghan kwa Umoja wa Mataifa (UN) umeunda "Kundi la Marafiki," linalosimamiwa na Uingereza na kujumuisha wawakilishi wa wanawake kwa UN na maafisa wakuu wa UN. Kundi hilo lilibuniwa kuwanusuru wanawake katika nyanja zote za maisha.

Ujumbe wa UN ndani ya Afghanistan (UNAMA) ulisema kupitia taarifa kwa vyombo vya habari mnamo Jumapili, 18 Novemba 2019 kwamba Kundi hili litaangazia umuhimu wa kulinda na kuboresha haki na dori ya wanawake ambayo wanaweza kucheza ndani ya mujtama na serikali kwa ujumla ikijumuisha juhudi za amani. Lengo la "Kundi la Marafiki" ni kuwawezesha na kutambua dori muhimu ya wanawake katika mustakbal wa Afghanistan. Malengo yao pia ni kuunnga mipango ya serikali ya Afghanistan na washirika wa kimataifa katika utekelezaji Maamuzi 1325 ya Baraza la Usalama la UN juu ya "Wanawake, Amani na Usalama." Adela Raz, Mwakilishi wa Kudumu wa UN ndani ya Afghanistan, alisema katika sherehe ya uzinduzi wa Kundi: *"Katika kipindi cha miaka 18 iliyopita, wanawake wa Afghan wamenyanyuka kama viongozi wa mabadiliko na wameanza kubadilisha hadithi kutoka kuwa ni waathiriwa na kuwa washirika. Ni sehemu ya hadithi yetu ya kufaulu, ni sehemu ya Afghanistan mpya, ambapo sote tunashirikiana ili kuhakikisha kuwa hakuna mwanamke anapigwa mawe hadi kufa; na kwamba anakatazwa kupewa elimu, na halazimishwi kubakia nyumbani. Ni wakati muhimu katika historia yetu ya kisiasa ambapo tumepanuka zaidi na uwekezaji wetu kwa wanawake wa Afghan lazima uendelee na uimarishwe."*

Kwa kuweka mipango hiyo, UN na wafanyikazi wake wanajaribu kuwaongoza wanawake wa Afghan kuamini kwamba kuna mustakbal mzuri ndani ya Afghanistan mpya. Kiasili ukweli uliochungu umefichika kwa wanawake na unawasilishwa kama ambaye wako njiani kuelekea kufaulu. Inawezaje kusemwa kwamba kuna kunyanyuka kwa ukweli kupitia tu serikali kuwapa viti baadhi ya wanawake ndani ya bunge au kuwapa baadhi nafasi ya kuingia katika soko la kisekula la ajira duniani au kuwaorodhesha baadhi yao kuwepo katika mashirika ya haki za wanawake; je yote haya ni kuionyesha dunia kwamba wanawake wa Afghan sasa wamekombolewa na kupata uhuru?

*Je ni vipi kuhusu vifo vingi (kuanzia 1 Januari hadi 30 Juni 2019, mzozo wa kisilaha umesababisha wanawake 430 kuwa waathiriwa (vifo 144 na 286 kujeruhiwa), ni kupungua kwa asilimia 22 ikilinganishwa na kipindi sawia mnamo 2018* ***UNAMA****), ukame (takribani wa Afghan milioni 5 wanauwezo mdogo au hawana kabisa wa kupata chakula,*
*Shirika la Chakula na Kilimo la* ***Umoja wa Mataifa****), ukosefu wa usalama wa kiuchumi na kiwango cha umasikini (asilimia 54 cha watu wanaishi ndani ya umasikini, wengi wao ni wanawake na watoto,* ***Shirika Kuu la Takwimu la Afghanistan****), maelfu ya wanawake ambao hawana elimu (asilimia 84 ya wanawake wa Afghan bado hawajui kusoma na kuandika na ni asilimia*

*Endelea Uk..9*

*mbili ya wanawake ambao wanapata nafasi ya elimu ya juu, **Shirika Kuu la Takwimu**), kuhangaishwa katika sehemu za kazi (asilimia 87 wamepitia kuhangaishwa katika sehemu za kazi na asilimia 91 ndani ya taasisi za elimu, **Wakfu wa Utafiti wa Sheria ya Wanawake na Watoto**), wajane (idadi ya wajane ndani ya Afghanistan inakadiriwa kuanza 600,000 hadi milioni mbili, moja ya viwango vya juu duniani, **Wizara ya Afghanistan ya Usimamizi wa Mambo ya Mujtama**), wanawake wanalazimishwa kuingia ukahaba na matumizi ya madawa ya kulevya (wako wanawake milioni 1 waliotekwa na madawa ndani ya Afghanistan, **Wizara ya Afya ya Ummah**), ufurushwaji wa wanawake (zaidi ya wa Afghan milioni 1.5 hivi sasa wamefurushwa kutokana na vita na mizozo, wengi wao ni wanawake na watoto, **Kitengo cha Kufuatilia Ufurushwaji wa Ndani**), wanawake ambao hawapati huduma muhimu (**zaidi ya asilimia 50 ya wanawake wajawazito ndani ya Afghanistan hawapati huduma muhimu, Wizara ya Afya Ummah**) na maelfu ya wanawake ambao wangelikimbia nje ya nchi lau wangelipata nafasi (karibia asilimia 50 ya wanawake wote wa Afghanistan wangeli kimbia nje ya nchi yao iliyokithiri vita lau wangeliweza, **taarifa za Wakimbizi**).*

Kwa hiyo nukta ambazo zimetajwa katika hotuba ya Adela Raz, Mwakilishi wa Kudumu wa UN ndani ya Afghanistan ziko kinyume na uhalisia wa Afghan wanawake. Wanawake wa Afghan sio viongozi wa mabadiliko na sio washirika bali ni waathiriwa wa mipango fisadi ya Amerika na serikali ya Afghan. Leo wanapigwa mawe hadi kufa lakini wanauliwa kwa mamia kwa vita vya utawala. Wao hawajakatazwa kupata elimu lakini serikali haiwajali na kuwapa fursa hii. Leo hawalazimishwi kubakia nyumbani bali maelfu ya wanawake wa Afghan lazima watoke nje ili kwenda kuombaomba ili kupata mkate wao wa siku. Je hiyo ndio dori ya wanawake ndani ya Afghanistan mpya?

Kwa kuongezea sehemu ya jamii ya kimataifa, Afghanistan imejifunga na matangazo, mikataba na maamuzi ya UN inayojumuisha kushughulikia haki za wanawake na wanadamu. Miongoni mwa hizi ni Maamuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 1325 (UNSCR 1325) na Makubaliano ya Kuondosha Aina Zote za Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake (CEDAW). “Kundi la Marafiki” linataka kunusuru utekelezaji wa mipango aina hiyo ambayo ni uhalifu mwingine dhidi ya wa Afghan wanawake kwa sababu mipango hii msingi wake ni mtazamo wa kidunia wa kisekula ambao unakwenda kinyume na maumbile ya Uislamu. Mipango yote hii inawasilisha kinadharia kwamba wanasimama nyuma ya usawa wa wanawake kushiriki katika kila nyanja ya maisha, wakitia mkazo kuzidisha idadi ya wanawake na kushiriki katika uongozi, kusitisha vurugu dhidi ya wanawake, kuwashirikisha wanawake katika michakato yote ya amani na usalama, kupanua uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kuufanya usawa wa kijinsia kuwa ndio suala kuu katika kupangilia na kujenga maendeleo ya kitaifa n.k… Lakini kivitendo, nukta hizi zinahusishwa na matatizo ya kiutekelezaji na hivyo mpaka sasa hakuna natija ya kufaulu kiukweli kunakoweza kuonekana ndani ya nchi yoyote na ndiyo maana wanawake bado wanapambana na ukosefu wa usawa katika saa za kufanyakazi, ajira na mishahara, umilikaji, kupendelea jinsia katika usambazaji wa elimu na afya, ukosefu wa usawa wa kijinsia katika uhuru wa maoni, ukosefu wa kijinsia kuhusiana na vurugu na kuathriwa n.k.

UNSCR 1325, CEDAW na mipango mingine sawia inaeneza sumu ambayo inawabadilisha wanawake wa mujtama kuwa watumwa wa matumizi na serikali za kisekula za kirasilimali. Wamo katika mzozo wa kudumu na wa kuchosha dhidi ya wanaume ili kwamba wasiwakandamize haki zao nao pia wanayo ruwaza kwamba mwanamume lazima daima awe anapata ridhaa ya mwanamke ili aweze kuwa na sura ya kisasa ya mwanamume aliyezindushwa na demokrasia.

Kiufupi, je imo ndani ya mipango hii ishara yoyote ya ulinzi, uhuru na usalama wa Afghan wanawake ambao “Kundi la Marafiki” jipya linataka kuinusuru serikali katika kuyatekeleza? Hakika hakuna!!! Yote haya ni ahadi tupu ambazo zimerudiwa kuwasilishwa kwa kipindi cha miaka 18 kwa sura mpya!

Ummah umepokea baraka kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), ambapo Mwenyezi Mungu (swt) ameupa suluhisho la matatizo yao yote. Badala ya kuweka nguvu katika miungano iliyofeli ya kidemokrasia na kupigania haki za wanawake zisizoweza kupatikana, wanawake Waislamu lazima wachukue suluhisho lililo tayari la Kiislamu. Uislamu umempa mwanamke haki ya kushiriki kisiasa, haki ya kusimamia mambo ya kiuchumi, haki ya kufanyakazi, haki ya kuhusishwa katika amali za kijamii, haki ya kupata kiwango cha juu cha elimu na karibia zote. Uislamu unampa mwanamke heshima, hadhi na usalama kama mwanadamu! Haki zote hizo zinaweza kudhaminiwa lau Shari’ah ya Mwenyezi Mungu (swt) inatawala. Hivyo basi, wanawake Waislamu wawekeze nguvu zao katika kunusuru kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume. Dola ambayo inawapa wao na wanawake wote duniani haki zao za kweli na hatimaye kuwatibu sumu ya demokrasia.

**[فَاحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنزَلَ اللّهُ وَلاَ تَتَّبِعْ أَهْوَاءهُمْ عَمَّا جَاءكَ مِنَ الْحَقِّ]**

“Basi hukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu wala usifuate matamanio yao ukaacha Haki iliyo kujia.” [al-Ma’idah: 48]

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Amanah Abed**

# S/J: Harakati za Kiraia Nchini Iraq, Lebanon na Iran

**Swali:**
Twajua kuwa harakati maarufu nchini Iraq, Lebanon na Iran zilianza kwa ghafla kama ilivyo dhihirika mnamo 5/11/2019; je, zingali hivyo? Je, kuna dori zozote za Ulaya katika nchi hizi tatu ambako Marekani ina ushawishi? Je, hali katika nchi hizi tatu itabaki kama ilivyo, au Marekani iko katika mchakato wa kuwabadilisha vibaraka hawa au baadhi yao kupitia mabadiliko ya kawaida au kupitia jeshi kama ilivyo fanya nchini Misri na Sudan? Mwenyezi Mungu akulipe kheri.

**Jibu:**
Ili kuliweka wazi jibu la maswali hayo ya juu, kwa kiasi fulani tutatathmini yafuatayo:

**Kwanza: Sababu na misukumo ya malalamiko hayo:**
Ndio, malalamiko hayo yalianza kwa ghafla katika nchi hizo tatu, na misukumo yake kwa mukhtasari ni kama ifuatavyo:

1- **Maandamano nchini Iraq:** Malalamiko yalizuka nchini Iraq mapema Oktoba 2019 kwa muundo wa maandamano na kufunga njia, yaliyo imarika na kuwa ufungaji wa madaraja jijini Baghdad na barabara kuu nyinginezo kulalamika dhidi ya kudorora kwa hali ya kiuchumi ya nchi hiyo, kuenea kwa ufisadi wa kiidara na kifedha katika taasisi za serikali na dhidi ya kukithiri kwa ukosefu wa ajira. Na maandamano hayo yalianza kwa ghafla baada ya kudhikika na kuadimika kwa nyenzo za riziki kwa watu. Serikali hiyo imeshindwa kutatua kadhia ya umeme katika umri wake wote wa miaka16, wala kutoa nafasi za kazi kwa vijana na wahitimu wa vyuo, wala kushibisha njaa ya watu licha ya kuwepo rasilimali kubwa za mafuta. Maandamano haya yakalipuka kwa kuuwawa karibu watu 350, ikiwemo kujeruhiwa na kukamatwa kwa maelfu. Afisi za vyama vinavyo unga mkono serikali ya Iran zilichomwa, na kisha kuwashwa moto eneo lililomo ubalozi wa Iran mjini Karbala mnamo 4/11/2019, wakiwarushia mawe, wakitaka watolewa mjini, na kuteketeza ubalozi wa Iran mjini Najaf mnamo 27/11/2019. Kilichoifanya serikali ya Iraq kutingishika na kushtuka zaidi ni kuwa maandamano haya yamezagaa miji ya Baghdad, Nasiriyah, Karbala, Najaf na miji mingineyo ya kusini; yale maeneo ambayo yalichukuliwa na serikali hiyo kuwa yenye ushawishi mkubwa. Athari yake ilikuwa mbaya sana hadi Abdul Mahdi akashindwa kuendelea kushikilia utawala, hivyo basi akajiuzulu mnamo 30/11/2019 na bunge kuidhinisha kujiuzulu huko mnamo 1/12/2019.

2- **Maandamano ya Lebanon:** Hali ya kiuchumi nchini Lebanon imefikia ukingo wa kuporomoka kabisa au inakaribia hilo! “Deni la umma la Lebanon mwanzoni mwa 2019 lilikuwa ni dolari bilioni 85.32” (Al-Arabi Al-Jadeed, 15/3/2019), na hili ni deni kubwa ambapo riba juu yake inakula takriban nusu ya mapato ya Lebanon. “Kiwango cha deni la nchi hiyo ikilinganishwa na uzalishaji jumla wa nchi ni asilimia 1.52, na riba juu ya deni hutumia takriban nusu ya mapato ya dola hiyo” (BBC 28/10/2019), na uhalifu huu mkubwa umeacha “kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira nchini Lebanon ukikadiriwa kuwa asilimia 37 kwa wale walio chini ya miaka 35 …” (BBC 26/10/2019). Usoni mwa maangamivu haya ya kiuchumi yaliyoletwa kwa watu na tabaka la kisiasa, cheche ya Ushuru wa WhatsApp mnamo 17/10/2019 iliwaka mabarabarani nchini Lebanon, na kuzichoma afisi hizo za manaibu hususan eneo la kusini mwa Lebanon na kuzighadhabisha Beirut, Nabatieh na Tyre, hivyo basi maandamano makubwa yakajitokeza. Na kisha kwa haraka yakaigeukia serikali kutaka ijiuzulu, na hata mabadiliko jumla ya viongozi wa kisiasa nchini Lebanon. Na kwa mawazo ya usalama ambayo dola na wafuasi wake nchini Lebanon wanayazalisha, wafuasi wa chama cha Iran walijaribu kuwatishia waandamanaji mnamo 24 na 25/10/2019 kwa kuvivamia viwanja, na kisha kurudiliwa na wafuasi wa chama cha Iran na Harakati ya Amal jijini Beirut!

3- **Maandamano ya Iran:** Serikali ya Iran haina ubora wowote kuliko dola muhimu kwake – Iraq, Lebanon na Syria kabla yao – kwa kuwa inakosa mtazamo wa kiuchungaji wa kusimamia nchi hiyo ambayo imepelekea Askari wa Mapinduzi kudhibiti sekta kubwa za uchumi wa Iran na kuyatelekeza maeneo yasiyo ya Kifursi pembeni ikisababisha msururu wa miji ya mateso pambizoni mwa dola hii na hali ya kiuchumi kukaribia kulipuka katikati na pembeni hali kadhalika na ilikuwa ni aibu kwa serikali hii kujigamba kwa mradi wa nuklia na makombora kwamba maandamano hayo maarufu yamelipuka kutokana na uhaba wa gasoline! Upungufu huu umetokana na ukosefu wa viwanda vya kusafisha mafuta, na viwanda vyepesi kwa nchi zinazojali vyema watu wake. Kisha, licha ya ongezeko la matumizi ya gasoline nchini Iran kwa takriban asilimia 40 tangu 2017 na kufeli kuendesha kiwanda cha usafishaji mafuta katika mkoa wa Hormuzjan, gasoline nyingi inaingizwa kwa magendo kutoka ng’ambo kwa sababu ya tofauti ya bei ya magenge ambapo sio vigumu kwa dola hiyo kugundua, ambalo ni dhihirisho jingine la kufeli kwa dola hiyo kusimamia rasilimali muhimu zaidi “mafuta”! Dola hiyo kisha ikapandisha bei ya gasoline kwa asilimia 300, na maandamano yakazuka mnamo 15/11/2019 jijini Tehran na miji kadhaa ya Iran. Maandamano hayo yaliongezeka, ambapo mabenki yaliteketezwa moto, majumba ya Wairani, afisi za usalama na serikali zilishambuliwa, na serikali kukata mtandao wa internet ili kuzuia mawasiliano miongoni mwa waandamanaji. Serikali ikaamua kufanya ghasia za kiwango cha juu zaidi katika kukabiliana na harakati hii ya maandamano na kuikandamiza kwa chuma na moto. “Majeshi ya usalama ya Iran yalipokuwa yakiendelea na msako wao wa waandamanaji, upinzani wa Iran, mnamo 23 Novemba idadi ya vifo vya maandamano hayo ilizidi watu 300, ili nakili majina 99 kati yao, na watu zaidi ya 4,000 walijeruhiwa, na zaidi ya watu 10,000 waliwekwa kizuizini, na ilionyesha kuwa Askari wa Maandamano

*Endelea Uk..11*



Email: info@uqab.or.ke

hayo walizitoa maiti kutoka mahospitalini hadi eneo lisilo julikana" (Arabic Independent 24/11/2019).

**Pili: Je, maandamano hayo yangali huru bila ya kuingiliwa kati na Ulaya?**
Ulaya imejaribu kuyapatiliza maandamano hayo kwa manufaa yake, lakini bado haijaweza kuwa madhubiti au kuwa na ushawishi katika kuupenya ushawishi wa Marekani katika nchi hizi tatu. Ufafanuzi huu ni kama ifuatavyo:

1- **Majaribio ya Ulaya nchini Iraq:** Kama tulivyo taja mwanzoni, maandamano nchini Iraq, hususan maeneo ya kusini, yalikuwa yanapamba moto, yaliyo makinika katika maeneo ya Kishia, na hauwezi kuondolewa uwezekano kuwa Ulaya hususan Uingereza, imejaribu kuyatumia maandamano haya, na ingawa hakujakuwa na dalili za kuaminika za Uingereza kuyaingilia maandamano hayo, Iran ilikuwa na tahadhari kuhusu jambo hili na hata ilikuwa imepagawa nayo kiasi ya kuwa khatibu wa Ijumaa wa Tehran Muhammad Ali Mouhadi Karma, alisema wakati wa khutba, akiwataja waandamanaji wa Iraq kama "Mashia wa Kiingereza", akiongeza "Baadhi ya makundi potevu tunayoyaita kama Mashia wa Kiingereza yamepenya ndani ya safu za watu wa Iraq …" (Iran International 11/11/2019). Taarifa yake ilikuwa kwamba maafisa wa Iran wanahofia kuwa Uingereza huenda ikapatiliza fursa ya harakati hizi za watu, mbali na Iran kujaribu kuwatishia waandamanaji kwa kuwatuhumu kuwa vibaraka wa Uingereza, hususan kwa kuwa msimamo wa Uingereza ulikaribia kuwa parwanja katika kuunga mkono maandamano hayo "Ubalozi wa Uingereza ulisema katika ukurasa wake rasmi wa mtandao wa Twitter kuwa "Maandamano ya amani ni haki ya watu wa Iraq." Alioongeza: "Ghasia dhidi ya waandamanaji hazikubaliki" … "Dua zetu ni kwa waliojeruhiwa na familia za wale waliopoteza maisha yao katika maandamano hayo." (Russian agency Sputnik 5/11/2019), ambao ni msimamo ule ule ulioonyeshwa na Waziri wa Kigeni wa Uingereza Andrew Morrison kama ilivyo nukuliwa na tovuti ya habari ya Al Ain mnamo 10/27/2019.

2- **Majaribio ya Ulaya nchini Lebanon:** Inajulikana kuwa wafuasi wa Marekani na Ulaya wanazunguka na kuzurura nchini Lebanon, na pia inajulikana kuwa wafuasi wa Marekani, ima moja kwa moja mithili ya Aoun na Berri au wasio moja kwa moja mithili ya Hezbollah kupitia Iran, ni upande ulio imara na wenye nguvu … Ama wafuasi wa Ulaya "Uingereza na Ufaransa" ni upande ulio dhaifu, kama vile Geagea na Jumblatt … Ama Hariri, ndiye aliye hatarini zaidi kwa sababu anatia mguu mmoja Ulaya na mguu mwengine kwa Saudi Arabia kibaraka wa Marekani, na wafuasi hawa hawawezi kutoa uamuzi, bali tu kufanya mambo yanayo ukanganya upande wa pili. Kwa mfano, mawaziri wa majeshi manne ya Lebanon mnamo 19/10/2019 walijiuzulu kutoka katika serikali ambayo waandamanaji wanataka kuiangusha, na Waziri Mkuu Saad Hariri akatangaza mnamo 18/10/2019 makataa ya masaa 72 kukabiliana na mgogoro huo, kisha akawasilisha kujiuzulu kwake mnamo 29/10/2019 dhidi ya matakwa ya kiongozi wa dola hiyo na matakwa ya chama kikuu cha usalama cha Iran nchini Lebanon. Kisha Ufaransa ikatuma mjumbe wake hadi Lebanon mkurugenzi wa Kitengo cha Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini katika Wizara ya Kigeni ya Ufaransa, Christophe Farno, "ambaye kwake – Raisi Aoun – alifikisha risala kutoka kwa Raisi wa Ufaransa Emmanuel Macron, na serikali ya Ufaransa ukithibitisha hamu ya Ufaransa katika hali nchini Lebanon na kutaka kwake kuisaidia Lebanon katika dhurufu za sasa" (Al-Arabia 11/11/2019). Ziara ya mjumbe huyo haikukubaliwa na wafuasi wa Marekani, kama Taasisi ya Kitaifa ya Habari Rasmi ilivyo mnukuu Waziri wa Kigeni Basil kuwa alimwambia mjumbe huyo wa Ufaransa: "Upande wowote wa nje usiwepo katika laini ya mgogoro wa Lebanon na kupatiliza kuutumia" … Uingereza pia ilituma mjumbe wake, Richard Moore, aliye kutana na Aoun na kusema: "Ufalme wa Uingereza daima umekuwa mshirika na msaidizi muhimu kwa Lebanon kwa muda mrefu, kwa mfano, mwaka jana uliwekeza $200 milioni ili kusaidia usalama, ustawi, ufanisi, na ubwana wa Lebanon." Aliendelea, "Ni muhimu kuendelea kuheshimu haki ya maandamano ya amani, na ukandamizaji wowote wa harakati hiyo ya maandamano kupitia ghasia au vitisho vya yeyote yule kamwe haikubaliki." (Arabic Independent 25/11/2019).

3- Majaribio ya Ulaya nchini Iran: Serikali ya Iran, kama kawaida, ilidai kuwa inajibu njama na matishio ya nje. "Leo, kinara wa Askari wa Mapinduzi ya Kiislamu y a Iran ametishia kuiangamiza Marekani, Israel, Uingereza, na Saudi Arabia, endapo zitavuka "mistari mekundu" katika kuamiliana na nchi yake. Salami alisema, katika hotuba iliyotolewa kwa waandamanaji wanaoiunga mkono serikali jijini Tehran na kupeperushwa na runinga ya Iran: "Naiambia Marekani, Israel, familia ya Saud na Uingereza mushawahi kushuhudia nguvu yetu katika uwanja wa vita na hamukuweza kukabiliana nayo; ulimwengu sasa umeyaona baadhi ya makofi yetu." Aliendelea: "Tunawaambieni: Musivuke laini zetu, lakini mukivuka mistari mekundu, tutawaangamiza" (RT 25/11/2019). Serikali hiyo inataka kuonyesha dhana kuwa nguvu za nje ziko nyuma ya maandamano hayo na sio kutoka kwa watu wenyewe walioonja uchungu. Zingatia kuwa viashiria vyote vyaonyesha kuwa maandamano hayo ya watu yanatoka ndani ya nyoyo na damu zao wenyewe! Lakini inaonekana kana kwamba sauti ya uingiliajikati kutoka nje inaendelea kuwepo ndani ya serikali ya Iran kiasi ya kuwa khatibu wa Ijumaa wa Tehran, kama tulivyotaja mbeleni, anawatuhumu Mashia wanao andamana nchini Iraq kuwa ni Mashia wa Kiingereza! Maandamano hayo nchini Iran sio ya mwanzo, wala hayatakuwa ya mwisho na labda yako huru na hayana dalili zinazoonyesha mikono ya kimataifa. Maandamano hayo nchini Iran, kama vile Syria, ni ya watu kupigana dhidi ya watawala madhalimu ambao sera zao hazijajua ladha ya mafanikio katika kuchunga mambo ya Ummah.

*Endelea Uk..12*

**Tatu: Ama kwa Marekani kubadilisha vibaraka wake katika nchi hizi tatu, jambo hili ni kama ifuatavyo:**

1- Ushawishi halisi katika nchi hizi tatu ni ushawishi wa Marekani, huku Ulaya (Uingereza na Ufaransa) zikiwa hazijafaulu katika kugawanya ushawishi huu pamoja na Marekani.

2- **Hadi Ummah utakapo nyanyuka kwa mapinduzi sahihi juu ya msingi wa Uislamu na kisha mabadiliko sahihi kutokea,** hadi hilo litokee, watawala wa nchi hizi tatu wataendelea kuwa chini ya sera ya Kimarekani kuwabadilisha au kuwabakisha.

3- Dola za kikoloni za kikafiri zinataka vibaraka hawa kutumikia maslahi yao. Ikiwa watu watapinga na kutakuwa na ghasia katika utawala wake, basi watampa muda maalumu; ikiwa hatawezi kuleta utulivu katika utawala, basi atakuwa ameshindwa kumtumikia bwana wake, hapo atambadilisha. Chombo cha hili ni urongo wa ile inayoitwa demokrasia kupitia kumleta kibaraka mpya asiyekuwa na sura nyeusi zaidi kuliko yule kibaraka aliyefurushwa; yaani, hii ni endapo mgogoro hautakuwa sugu, lakini endapo utakuwa sugu chombo kitakuwa ni "jeshi" kama ilivyofanya nchini Misri 2011 au Sudan 2019.

**Nne: Kutathmini mabadiliko tarajiwa katika nchi hizi tatu kwa mujibu wa uhalisia wa sasa, yafuatayo ndio yaliyo dhahiri:**

1- **Kuhusiana na Iran:** Marekani inatangaza waziwazi kuwa haitaki kubadilisha serikali nchini Iran; yaani, kadri mauwaji yatakavyokuwa katika maadamano hayo, Marekani inaamini kuwa serikali hii ingali inatumikia maslahi yake! Katika wakati ambapo damu ya Waislamu nchini Iran ilimwagwa na serikali hiyo, maafisa wa Marekani walikuwa wakisisitiza juu ya kudumishwa utulivu "afisa mkuu wa ikulu ya White House alisema Jumapili kuwa nchi yake haitaki kubadilisha serikali nchini Iran…" (Al Arabiya Net Jumapili, 11/17/2019); hivyo basi, hakuna mabadiliko yanayo tarajiwa katika serikali ya Iran kutokana na maandamano hayo ya 11/2019 kama vile ambavyo hakukuwa na mabadiliko kutokana maandamano ya mwaka jana.

2- **Kuhusiana na Lebanon:** Kama tulivyo taja, Lebanon ina wafuasi wa Marekani na wafuasi wa Ulaya, timu ya kwanza ndio yenye nguvu zaidi na hii ndio inayoendesha hali ya madhaifu kwa mujibu wa njia ya maridhiano, na pande hizo mbili zinatofautiana juu ya serikali ya kiufundi na kisiasa au serikali ya kitaalamu! Baada ya yote haya, inatarajiwa kuwa Marekani itabadilisha mizani ya serikali nchini Lebanon, ili ushawishi uwe kwa wafuasi wa Marekani na kuwahusisha wafuasi wa Ulaya lakini kwa kiasi fulani, kisha kuzihusisha barabara ili kuzituliza.

3- **Kuhusiana na Iraq:** Marekani inaitawala Iraq karibia moja kwa moja nyuma ya pazia. Ubalozi wake jijini Baghdad una wafanyikazi 16,000, wanao fuatilia kazi ya mawaziri wote wa Iraq, hususan sekta za mafuta na usalama, na ndio ubalozi mkubwa zaidi wa Marekani duniani. Ina kambi nyingi za kijeshi nchini Iraq, maarufu zaidi katika hizo ni kambi ya Ain al-Assad mjini Anbar. Katika wiki ya mwisho ya mwezi uliopita, Marekani ilizidisha ujumbe wake, hivyo ziara ya ghafla ya Makamu wa Raisi wa Marekani Pence mnamo 23/11/2019 katika kambi ya Ain al-Assad, na kabla ya wiki kumalizika ya ziara ya Makamu wa Raisi wa Marekani nchini Iraq, Marekani ilimtuma kamanda wa Muungano wa Wakuu wa Kijeshi wa Jeshi la Marekani Mark Milley hadi Baghdad mnamo 27/11/2019. Hii ni dalili ya kudumu kwa ufuatiliaji wa Marekani hususan kwa kuwa Iraq ni kesi tete kwa Marekani; iliivamia na kudai kuwa inaishika mkono katika maendeleo lakini ikaipeleka katika ghasia na maangamivu, na sasa iko katika msururu wa migogoro na inatarajiwa kuwa endapo hali hazitakuwa shwari karibuni Marekani italeta mabadiliko kupitia "jeshi" na kuzihusisha barabara pamoja nao katika kutawala kama ilivyo fanya nchini Misri au Sudan. Imeoneka kuwa vyombo vya Kupambana na Ugaidi nchini Iraq, ambalo ni jeshi kubwa lililo undwa na Wamarekani na kupewa zana bora zaidi za kijeshi; viko mbali sana na sera ya kuyazima maandamano hayo, na inaonekana kuwa waandamanaji katika Uwanja wa Tahrir wanalitazama jeshi hili kama mkombozi wao kutokana na wanasiasa wafisadi kwani wanabeba picha ya Jenerali Abdel-Wahab Al-Saadi, mmoja wa viongozi wa taasisi hiyo baada ya kufutwa kazi na Abdel-Mahdi kana kwamba jeshi hili linakubaliwa na waandamanaji hao kuwa na dori ya kupangilia suluhisho. Hii ni upande mmoja, huku upande mwengine, mikutano ya kijeshi iliyo fanywa na Marekani jijini Baghdad, na kupeleka wajumbe wake kwa ajili ya hilo ikiongezewa na kazi ya ubalozi wake mkubwa jijini Baghdad, yote haya ni matayarisho ambayo Marekani inayatayarisha pindi yatakapo hitajika.

Hili halitaathiriwa na kujiuzulu kwa Abdel-Mahdi na kuteuliwa kwa raisi mpya, kwani hili halitatui tatizo hilo, bali ni la muda tu, ikiwa na maana kuwa kidonda kitabakia wazi hadi kipone!

Lakini, harakazi kubwa katika nchi hizi tatu zina nukta za kuungwa mkono na nukta za kupingwa. Ama nukta za kuungwa mkono kwake ni kuwa harakati hizi ziko huru, na kwa kiasi kikubwa zingali huru. Ama nukta zinazo pinga dhidi yake ni kuwa bado hazijachukua uongozi wenye ikhlasi kwa Mwenyezi Mungu Subhanahu, na ikhlasi kwa Mtume Wake, rehma na amani zimshukie na jamaa zake, ili kuangaza njia yake kwa utawala wa Uislamu, Khilafah Rashida ya kweli. Na endapo harakati hizi zitaendelea pasina uongozi wenye ikhlasi na hivyo kuendelea pasi na uongofu, basi juhudi na kujitolea kwake zitaambulia patupu, na harakati hiyo hatimaye itakuwa mithili ya yule aliye geuza mwelekeo wake baada ya kuwa na nguvu! Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuongoza katika njia sahihi.

7 Rabii' II 1441 H
04/12/2019 M